
# Masimulizi






BIBLIA INATUSIMULIA KUHUSU MUNGU. MASIMULIZI YA MUNGU
HAPO MWANZONI – HATA KABLA YA DAHARI – MUNGU ALIKUWEPO
YEYE MUNGU.... NDIYE ALIYEUMBA MBINGU NA NCHI TUNAYOIONA SASA.
NA MUNGU AKASE-MA, “NA UWEPO MWANGAZA,” NA MWANGAZA UKAWA
AKAUTENGANISHA MWANGAZA KUTOKA KWA GIZA IKAWA JIONI NA ASUBUHI – SIKU YA KWANZA.
MUNGU AKAUMBA ANGA NA KUYATENGA MAJI YA CHINI YA ANGA NA YA JUU YA ANGA NA KUIITA ANGA “MBINGU.”
HII NDIO SIKU YA PILI YA UUMBAJI



MUNGU AKASEMA, “NA IWE KWAMBA MAJI YALIYO CHINI YA MBINGU YAKUSANYIKE MAHALI PAMOJA, NA UDONGO UONEKANE.”
MUNGU AKAIITA UDONGO NCHI NA MAJI AKAYAITA ‘BAHARI.”
MUNGU AKANENA NA UDONGO UKACHIPUZA MIMEA: MICHE ILIYOKUWA NA MBEGU SAWASAWA NA ASILIA YAKE NA MITI ILIYOZAA MATUNDA YALIYO NA MBEGU NDANI YAKE.
HII NDIYO ILIKUWA SIKU YA TATU YA UUMBAJI.

SIKU YA NNE MUNGU ALISEMA, NA KUWEPO NA MIANGA KATIKA ANGA YA MBINGU ILI KUTENGANISHA MCHANA NA USIKU, NA IWE KAMA ISHARA YA KUKADI-RIA MISIMU, SIKU, NA MIAKA NA ITOE MWANGAZA KATIKA UPANA WA ANGANI NA KUTOA MWANGAZA DUNIANI.”
KWA HIVYO SIKU YA NNE MUNGU ALIUMBA MBINGU, JUA, MWEZI NA NYOTA.



SIKU YA TANO MUNGU AKASEMA," MAJI YAJAE VIUMBE WENYE UHAI, NA NDEGE WAPAE ANGANI."
MUNGU ALIWAUMBA VIUMBE WAKUU WA BAHARINI NA KILA CHENYE UHAI MAJINI NA KILA NDEGE ANAYE PAA ANGANI KILA MMOJA KWA JINSI YAKE.
GOD AKAWABARIKI NA KUWAAMBIA WAONGEZEKE WAJAZE BAHARI NA NDEGE WAONGEZEKE NCHINI.



SIKU YA SITA MUNGU AKASEMA, "WACHA NCHI ITOE VIUMBE VILIVYO HAI, MIFUGO, VIUMBE VINAVYOTAMBAA, NA WANYAMA WA PORINI KILA MMOJA KWA JINSI YAKE.
KWA HIVYO, SIKU YA SITA MUNGU ALIWAUMBA WANYAMA WOTE.


SIKU IYO HIYO MUNGU ALIKIUMBA KIUMBE KINGINE KUTOKA KWA MAVUMBI.
AKAKIPULIZIA UZIMA KIKAFANYIKA KUWA NAFSI INAYOISHI.
MUNGU AKAKIITA HICHO KIUMBE “MTU” NA KUKIITA ÄDAMU.”
MUNGU AKAIANGALIA KAZI YAKE YA UUMBAJI NA KUSEMA, “NI NZURI SANA.”
AKAMPATIA MTU PARADISO – ILIKUWA BUSTANI ILIYOITWA ”EDENI.”
MUNGU AKAMPATIA MTU KAZI YA KUFANYA – KULITUNZA SHAMBA.


KATIKATI YA BUSTANI MUNGU ALIUPANDA MTI WA UZIMA – AMBAO ULILETAUZIMA WA MILELE. PIA ALIUPANDA MTI MWINGINE – MTI WA MAARIFA YA KUJUA MEMA NA MABAYA.
MUNGU AKAMWAMBIA MTU YA KUWA ANGEKULA TUNDA LOLOTE KUTOKA KWA MTI WOWOTE – ILA ALIMPA ONYO…
USILE TUNDA LA MTI WA MAARIFA YA KUJUA MEMA NA MABAYA, UKIFANYA HIVYO NAKUHAKIKISHIA, UTAKUFA.


MUNGU AKAMLETEA ADAMU WANYAMA WA NCHINI NA NDEGE WA ANGANI ILI AWAPE MAJINA.


YULE BINADAMU WA KWANZA ALIKUWA NA UHUSIANO WA KARIBU SANA NA MUNGU
LAKINI MUNU ALIJUA YA KUWA SIO VYEMA ADAMU AWE MPWEKE.
AKAMFANYA ALALE USINGIZI – NA ALIPOLALA MUNGU AKACHUKUA MOJAWAPO YA UBAVU WAKE.

NA KUTOKA KWA UBAVU HUU AKAMUUMBA MWANAMKE WA KWANZA…
AKAMLETEA ADAMU…
ADAMU AKAMWITA MKEWE “HAWA.” AMBAYE NDIYE MAMA WA BINADAMU WOTE.
WALIKUWA BUSTANINI PAMOJA, DAIMA KWA FURAHA.


LAKINI KUNA KIUMBE KINGINE KILICHOTAKA KUWAZUIA BINADAMU WASIDUMU KATIKA FURAHA YA BWANA.
LUSIFERI (SHETANI) – MALAIKA ALIYEMUASI MUNGU NA KUFURU-SHWA KUTOKA MBINGUNI.
ALIMJIA ADAMU NA HAWA KATIKA BUSTANI AKIWA KWA MFANO WA JOKA.
JE NI KWELI MUNGU ALISEMA, “MSILE TUNDA LOLOTE SHAMBANI?”
TUNAO UHURU WA KULA TUNDA LOLOTE KATIKA BUSTANI HII – ILA TU TUNDA LA MTI ULIO KATIKATI YA BUSTANI.
HATUFAI HATA KULIGUSA, LA SIVYO TUTAKUFA.
LA. HAMTAKUFA. MUNGU ANAJUA, MKILIKULA HILO TUNDA, MTAKUWA JINSI YEYE ALIVYO, MKIYAJUA MEMA NA MABAYA.
WOTE WAWILI MUME NA MKE WALIKULA TUNDA LILE WALILOKATAZWA NA MUNGU, NA MATOKEO YAKE…


DHAMBI ILIINGIA ULIMWEN-GUNI KUPITIA KWA KUTOTII KWAO. HIVYO SASA WAKAJITAMBUA YA KUWA WALIKUWA UCHI – WAKAINGIWA NA HOFU.
LAKINI HATA HIVYO, DHAMBI ILIPOINGIA DUNIANI KWA MARA YA KWANZA, MUNGU NDIYE ALIYETOA DHABIHU.
ALIWATENGENEZEA NGUO ZA NGOZI ILI KUUFUNIKA UCHI WAO NA PIA DHAMBI ZAO. KISHA AKAWAONDOA SHAMBANI ADAMU NA HAWA.
LAKINI ALIAHIDI YA KUWA BAADAYE KUTATOKEA MKOMBOZI AMBAYE ATAMSHINDA SHETANI.
KUTAKUWEPO NA UADUI KATI YAKO NA MWANAMKE NA KATI YA UZAO WAKO NA UZAO WAKE.
ATAKUPONDA KICHWA NAWE UTAMPIGA KISIGINO.
ILI KUHAKIKISHA YA KUWA BINADAMU HAWARUDI TENA KATIKA BUSTANI, MUNGU ALIMWEKA MALAIKA KATIKA LANGO LA SHAMBA ILI KUILINDA NJIA YA KWENDA KWA MTI WA UZIMA.


IDADI YA WATU ILIZIDI KUONGEZEKA, DUNIA IKAJAA UOVU. MUNGU AKAHUZUNISH-WA SANA NA DHAMBI ZA WATU NA MAASI YAO.
IDADI YA WATU ILIZIDI KUONGEZE-KA, DUNIA IKAJAA UOVU. MUNGU AKAHUZUNISHWA SANA NA DHAMBI ZA WATU NA MAASI YAO.
LAKINI MTU MMOJA ALIPATA KIBALI MACHONI PA MUNGU. MUNGU AKAMWAMBIA NUHU AJENGE SAFINA.
AKAMLETEA WAWILI WAWILI WA KILA AINA YA MNYAMA ILI WAINGIE KATIKA SAFINA.
MUNGU AKALETA GHARIKA KUU DUNIANI NA KILA KIUMBE CHENYE UHAI AMBACHOHAKIKUINGIA KATIKA SAFINA KILIANGAMIA.
MUNGU AKAWAKOMBOA WAWILI WAWILI WA KILA AINA YA MNYAMA, NUHU NA JAMII YAKE.
MUNGU AKAMWAMBIA NUHU NA JAMII YAKE, "ZAENI MATUNDA, MUONGEZEKE KWA IDADI NA MUUJAZE ULIMWENGU."
HII JAMII MOJA NDIO CHANZO CHA JAMII ZA MATAIFA YOTE YA ULIMWENGUNI.
LAKINI PIA, WATU WALIAMUA KTOMTII MUNGU.


MUNGU AKAWAAMBIA WATU WAUJAZE ULIMWENGU NA WAONGEZEKE. LAKINI HAWAKUITII AMRII YA MUNGU.
BADALA YA KUTII NA KUSAMBAA ULIMWENGUNI WALIVYOAMRISHWA NA MUNGU, WALIAMUA KUKAA KATIKA NCHI TAMBARARE YA BABELI.
WAKAANZA KUJENGA MNARA MKUU ILI KUJITENGENEZEA JINA BADALA YA KUMTII MUNGU.
HATUHITAJI KUTAWALIWA NA MUNGU. TUTAJIJENGEA MJI MKUU NA MNARA PAPA HAPA.
KIONGIZI WAO ALIITWA NIMRODI NAYE AKAWAHIMIZA WAASI.
LAKINI MUNGU ALISHUKA PALE KWA MNARA WA BABELI AKAWACHAFULIA USEMI WAO.
BADALA YA LUGHA MOJA, WALINENANA KWA LUGHA NYINGI TOFAUTI TOFAUTI; NA WLIONENA KWA LUGHA SAWA WLIFUNGA SAFARI NA KUSAFIRI PAMOJA.


MPANGO WA MUNGU WA UKOMBOZI ULIANZA WAKATI ALIPOMCHAGUA MTU MMOJA – ABRAHAMU. MUNGU ALIMWAHIDI…
"NITAKUFANYA UWE TAIFA KUU."
MUNGU AKAMWAHIDI UZAO WENYE IDADI KUBWA KAMA VILE NYOTA ZA ANGANI.
MMOJA WA UZAO WANGE NDIYE ANGEFANYIKA KUWA MKOMBOZI WA ULIMWENGU.
ABRAHAMU ALIPOHITIMISHA MIAKA MIA MOJA, ALIMZAA MWANA JINSI ALIVYOAHIDIWA NA MUNGU.
LAKINI MUNGU AKAMJARIBU ABRAHAM.
"MCHUKUE MWANAO UMTOE KAMA DHABIHU YA KUTEKETEZWA."
ABRAHAMU ALITII – AKIAMINI YA KUWA MUNGU ATAMFUFUA MWANAWE KUTOKA KWA WAFU.
ALIPOKUWA TU, KARIBU KUMWANGA-MIZA MWANAWE…
"ABRAHAMU! USIMDHURU.."
AKATAZAMA NA KUONA MWANAKONDOO KICHAKANI AMENASWA KWA PEMBE ZAKE AMBAYE NDIYE WA KUTOLEWA DHABIHU KWA MUNGU.
"HIVI SASA NAJUA UNANIPEN-DA KWA KUWA HUJANIZUILIA MWANAO."
ABRAHAMU NA MWANAWE WAKAITOA DHABIHU AMBAYO MUNGU ALIWAJALIA.



IDADI YA WAZAWA WA ABRAHIMU IKAZIDI KUONGEZEKA, JINSI VILE ALIVYOAHIDI MUNGU.
KUKAWA NA BAA LA NJAA, NAO WAKAHAMIA NCHI YA MISRI WALIKOZIDI KUONGEZEKA.
WALIPOKUWA NCHINI MISRI, WALINYANYASWA NA KUGAN-DAMIZWA NA KIONGOZI WA MISRI.
LAKINI WAKATI UNAOFAA ULIPOWADIA, MUNGU AKAMLETA MUSA ILI AWAON-GOZE KUTOKA MISRI.
MUNGU ALIFANYA MIUJIZA MINGI MIKUU YA KUONYESHA YA KUWA YEYE NDIYE ANAYEWAONGOZA KWENDA KWA NCHI YA AHADI ALIVYOMWAHIDI ABRAHAMU.
MUNGU AKAWAPA SHERIA – AMRI KUMI BAADHI YA NYINGINEZO, JINSI YA KUMPENDA MUNGU NA MAUSIANO BAINA YA WATU.
PIA AKAWAONYESHA NAMNA YA KUABUDU NA KUTOA DHABIHU KAMA KIASHIRIO CHA KUWAKUM-BUSHA DHAMBI ZAO.
USIWE NA MIUNGU MINGINE ILA MIMI.
USIJIFANYIE SANAMU Y A AINA YOYOYTE.
USILITAJE BURE JINA LA BWANA, MUNGU WAKO.
IKUMBUKE SIKU YA SABATO UITAKASE.
WAHESHIMU BABA YAKO NA MAMA YAKO.
USIUE.
USIZINI.
USIIBE.
USISHUHUDIE UONGO.
USIKITAMANI CHOCHOTE ALICHO NACHO JIRANI YAKO.



MUNGU AKAWAREJESHA KATIKA NCHI ALIYOMWAHIDI ABRAHAMU.
HATA INGAWA WATU WA MUNGU WALIMWONA MUNGU AKIFANYA MIUJIZA TENA NA TENA – BADO HAWAKUTII AMRI ZAKE.


WALIABUDU MIUNGU NA KUTENDA DHAMBI.
HAYA WALIYAFANYA KWA MDA MREFU.
WATU WENGI WAKASEMA YA KUWA HAWAKUTAKA KUITII SHERIA YA MUNGU ALIYOILE-TA KUPITIA KWA MUSA.


BAADHI YA VIONGOZI NA WAFALME WAO WALIMPENDA NA KUMFWATA MUNGU. NAO WALITENDA MAKUU…



….HATA KUUWA MAJITU.


WAFALME WENGINE WALIAMUA KUABUDU MIUNGU WA UONGO NA KUWAFANYA WATU WAABUDU SANAMU.
LAKINI KWA SABABU ALIWAPENDA – MUNGU ALIWATUMA MANABII KWA WATU WAKE.
WATU WALIOTUMWA NA MUNGU ILI WAWAFUNZE KUMPENDA MUNGU NA KUWACHA KUTENDA MABAYA.


WATU AMBAO MUNGU ALICHAGUA KAMA MWONGOZO WA KUULETA ULIMWENGU KWAKE WALIWAPUUZA MANABII – HATA INGAWA ALIWATU-MA TENA NA TENA.
HATIMAYE – MUNGU AKAMTUMA MFALME MDHALIMU NA JESHI LAKE WAKAUHARIBU MJI WAO NA HEKALU WALIMOMWABUDU MUNGU.

KWA MIAKA 70 WATU WA KIPEKEE WA MUNGU WALIKUWA MATEKA KATIKA NCHI YA KIGENI KAMA ADHABU YA DHAMBI ZAO ZA KUMKATAA MUNGU NA AMRI ZAKE.

LAKINI JINSI ALIVYOAHIDI, MUNGU ALIWAREJESHA BAADA YA MIAKA 70.
KATIKA KIPINDI HIKI, MUNGU ALIZIDI KUWATUMA MANABII NA WAALIMU WA KUWAELEZA JINSI YA KUISHI.



HALAFU KUKAWA NA KIPINDI CHA MIAKA 400 CHA KIMYA. WAKATI HUU MUNGU HAKUMTUMA NABII YEYOTE.
KATIKA HII MIAKA 400 UTAWALA WA KIYUNANI CHINI YA UONGOZI WAKE JEMEDARI ALEKSANDA ULIENEA NA KUTAWALA SEHEMU KUBWA YA MASHARIKI YA KATI, MAHALI AMBAPO WATU WA MUNGU WALIISHI.
HALAFU BAADAYE, SERIKALI YA KIRUMI IKAJA MAAMLAKANI NA KUWATAWALA WAYUNANI, ISRAELI NA MATAIFA MENGINE.
LAKINI WAKATI HUU KATIKA HISTORIA…
…MUNGU AKATUMA DHABIHU KAMILIFU ULIMWENGUNI.
DHABIHU HII HAINGEKUWA KAMA DAMU YA MBUZI NA NG'OMBE AMBAYO WATU WALIKUWA WAKITOA KWA AJILI YA DHAMBI ZAO.
HII ILIKUWA DHABIHU YAKE MUNGU – DHABIHU YA KIUNGU YA KUONDOA DHAMBI ZOTE ZA ULIMENGU
MUNGU HAKUWASAHAU WATU WAKE.


TANGU MWANZO, KILA MTU ALITENDA DHAMBI NA KUAMBUKIZWA MAKOSA.
NDIO MAANA MUNGU ALILETA ULIMENGUNI DHABIHU AMBAYO HAINA KOSA LOLOTE.
MTU AMBAYE HANA DHAMBI YOYOTE YA WATU.
MUNGU ALIILETA HII DHABIHU KWA NJIA YA KIPEKEE.
ALIMCHAGUA MWANAMKE MMOJA – BIKIRA ASIYEMJUA MWANAMUME – ILI BABAKE ASIWE BINADAMU MWENYE DHAMBI.
ROHO MTAKATIFU WA MUNGU AKAMSHUKIA HUYO BINTI, MARIA, NAYE AKACHUKUA MIMBA.
MIMI NI MTUMISHI WA MUNGU, NA YAFANYIKE ULIVYOSEMA.
KUZALIWA KWA HUYU MTOTO SPESHELI HATA KULITANGAZWA NA MALAIKA.
UTUKUFU KWA MUNGU JUU MBINGUNI, NA DUNIANI; AMANI KWA WATU WOTE WALIO NA KIBALI CHAKE.
HUYI MTOTO ALIPEWA JINA YESU – ALIKUWA MWANA WA MUNGU.



ALIKUWA MTOTO WA KIPEKEE AMBAYE HATA ALIPOKUWA KIJANA, ALIKUWA MJUZI NA HATA ALIWAFUNZA VIONGOZI WA DINI.
WAKATI UNAOFAA ULIPOFIKA, AKABATIZWA NA KUANZA KUTIMIZA SEHEMU YAKE KATIKA HISTORIA – KUWAFUMBULIA WATU JINSI MUNGU ALIVYO – NA KUWA YEYE NDIYE DHABIHU YA DHAMBI ZA WATU.
SHETANI AKATOKEA TENA, JINSI ALIVYOWATOKEA ADAMU NA HAWA, KUWASHURUTISHA WATENDE DHAMBI NA KUFWATA NJIA ZAKE BADALA YA NJIA ZA MUNGU.
NITAKUPA HIZI MILKI ZOTE ZA ULIMWENGUNI NA UTUKUFU WAKE IWAPO UTANIABUDU.
UMWABUDU BWANA MUNGU WAKO NA UMTUMIKIE YEYE PEKEE.
YESU AKAANZA KUWAFUNDISHA WAUME NA WAKE, VIJANA NA WASICHANA JINSI MUNGU ALITAKA WAISHI.
WAMEBARIKIWA WENYE HURUMA, KWA MAANA WATAHURUMIWA.
WAMEBARIKIWA WENYE MOYO SAFI KWA MAANA WATAMWONA MUNGU.
WAMEBARIKIWA WANAOTAFUTA AMANI KWA MAANA WATAITWA WANA WA MUNGU.


YESU ALIPOKUWA DUNIANI ALIWAONYE-SHA WATU JINSI YA KUMFWATA MUNGU NA KUWAPENDA WATU.
UNACHOMTENDEA MMOJAWAPO WA HAWA WADOGO UMENIFANYIA MIMI.
IWAPO UMENIONA, UMEMWONA BABA.
PIA AKATUFUNULIA JINSI ALIVYO MUNGU.
ALIWALISHA WATU.
ALIWAPONYA WATU.
ALITEMBEA JUU YA MAJI.
AAM!!
KIJANA YU HAI…
HATA ALIWAFUFUA WAFU.
NI MUNGU ANA UWEZO WA KUFANYA MUUJIZA KAMA HUU!!


ALIWAPENDA NA KUWABARIKI WATOTO.
AKAWAARIFU WATU KUHUSU MBINGUNI.


AKAWAELEZA KUHUSU JEHANAMU.
TAFADHALI MTUME LAZARO ATIE KIDOLE CHAKE MAJINI HALAFU ANIGUSE ULIMI!
MTUME LAZARO KWA NDUGU ZANGU…
…AWATAHADHARISHE DHIDI YA HAPA MAHALI PA DHIKI.


HATA ALIFUKUZA MAPEPO KUTOKA KWA WATU.
KATIKA KILA NJIA ALIJIDHI-HIRISHA KUWA MUNGU.


KUSEMA KWAKE KUWA AIKUA MUNGU KULIWAKA-SIRISHA SANA VIONGOZI WA DINI.
AKASHTAKIWA KWA MAKOSA YASIYO YA UKWELI.
ALIPIGWA MIJELEDI NA KUSULUBISHWA MSALABANI.
ALIKOKUFA
BABA – POKEA ROHO YANGU.
SHETANI, VIONGOZI WA DINI, WARUMI NA DHAMBI ZETU ZILICHANGIA PAKUB-WA KUMWUUA YESU.
WALIFIKIRI YA KUWA WAKIM-WUUA WATKUWA WAMEFAULU KUUZIMA UJUMBE WAKE NA MADHUMUNI YA MUNGU.
LAKINI WALIKOSEA…
WALITIMIZA TU MIPANGO YA MUNGU – TANGU MWANZO – KATIKA BUSTANI.
KUMPATANISHA MUNGU NA WATU KWA KUTOA DHABIHU KAMILIFU YA KUONDOA DHAMBI
YESU NDIYE ILE DHABIHU KAMILI ISIYO NA DHAMBI HASWA MWANA WA MUNGU.
AKADHIBITISHA KWA KUFUFUKA KWA WAFU.


BAADA YA KIFO CHAKE YESU, YESU ALIWAONEKANIA WAFWASI WAKE.
NA KUWAPA MAAGIZO, WAENDE WAWAAMBIE WENGINE KUHUSU MANENO YAKE, MAISHA YAKE – NA HATA KUFA NA KUFUFUKA KWAKE.
ENENDENI KWA MATAIFA YOTE MUWAFANYE KUWA WANAFUNZI WANGU, MUWABA-TIZE KWA JINA LA BABA NA LA MWANA NA LA ROHO MTAKATI-FU, MKIWAFUNZA KUTII AMRI ZANGU ZOTE KWENU.
NA, HAKIKA NIKO NANYI DAIMA, HATA MWISHO WA DAHARI.
YEYOTE ATAKAYE LIITA JINA LA BWANA ATAOKOLEWA.
NATAKA KULIITA JINA LA BWANA!
YESU!
MIMI PIA!
ALIPOONDOKA DUNIANI WAFWASI WAKE WALIFANYA HIVYO – NA WATU WENGI WAKAAMINI.
YESU ALISEMA ATARUDI DUNIANI KUWACHUKUA WOTE WANAOMPENDA NA KUMFWATA.
ATAKAPORUDI, PARADISO ITAREJESHWA TENA.
WATU, WANYAMA, NA VITU VINGINE TULIVYOVIPENDA VITAKUWEPO.
KUTAKUWEPO NA MBINGU MPYA NA NCHI MPYA.
WATU WOTE, WAZEE KWA VIJANA WALIOMFWATA YESU WATAKU-WEPO – MILELE.
JE, WEWE UTAKUWEPO?




# NITAMJUAJE MUNGU KWA KUMFWATA YESU?

## FWATA HATUA ZIFWATAZO:

1. MWAMBIE YESU YA KUWA UNAJUTIA MABAYA YOTE ULIYOYATENDA NA UMJULISHE YA KUWA UNATAKA KUBADILI MWENENDO WAKO UMFWATE YEYE.
2. UMWOMBE MSAMAHA NA UMWAMBIE YA KUWA UNATAKA KUMFWATA MAISHA YAKO YOTE.
3. UMSHUKURU KWA KUKUSIKIA NA KUYAJIBU MAOMBI YAKO.
4. SOMA BIBLIA KILA SIKU – MAMBO YA MUNGU.
5. MWAMBIE MTU ANAYEMPENDA YESU KUHUSU HATUA ULIZOCHUKUA NA MUANZE KUKUTANA WENZAKO WANAOMPENDA YESU KWA VIKUNDI.



Hii Hadithi imenukuliwa kutoka kwa Biblia ya Kingstone, inayochapishwa na Kingstone Comics.